JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2021

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2021

# 01 KISWAHILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ........................................ 2

2.1 Sehemu A: Imla ........................................................................................ 2
2.2 Sehemu B: Umoja na Wingi ........................................................................ 8
2.3 Sehemu C: Methali ........................................................................................ 14
2.4 Sehemu D: Matumizi ya Alama za Uandishi ........................................ 20
2.5 Sehemu E: Ufahamu ........................................................................................ 25

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ........................................................................................ 32

4.0 HITIMISHO ........................................................................................ 33

5.0 MAPENDEKEZO ........................................................................................ 34

KIAMBATISHO CHA PEKEE ........................................................................ 36

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2021. Taarifa hii inachambua majibu ya maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Kiswahili. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu sababu zilizochangia ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili. Aidha, taarifa hii inaonesha jinsi ufundishaji na ujifunzaji ulivyomwezesha au kushindwa kumwezesha mwanafunzi kupata maarifa stahiki kwa kipindi cha miaka minne.

Taarifa hii imechambua sababu mbalimbali zilizochangia baadhi ya wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa ufasaha. Baadhi ya sababu hizo ni kushindwa kutambua matakwa ya swali, kukosa maarifa kuhusu swali husika na athari ya lugha mama. Mtawanyiko wa majibu ya wanafunzi kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi kwa kutumia vielelezo, chati na maelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, taarifa hii itawawezesha wanafunzi na wasimamizi wa elimu kubuni mbinu zitakazosaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa lengo la kukabiliana na changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa, maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi, yatasaidia kuongeza umahiri wa wanafunzi na hatimaye kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa nchini.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inatoa mrejesho wa namna ambavyo wanafunzi walijibu maswali katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Kiswahili kwa mwaka 2021. Upimaji huu ni wa nne katika muhtasari wa mwaka 2015 unaozingatia kuimarisha umahiri kwa mwanafunzi katika stadi za kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika.

Upimaji wa somo la Kiswahili ulikuwa na sehemu tano. Sehemu A ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kusikiliza matamshi ya silabi, maneno, sentensi na kuyaandika (imla). Sehemu B ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kutumia maumbo ya umoja na wingi wa maneno katika mawasiliano. Sehemu C ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kutumia methali na kuelewa maana zake katika lugha ya Kiswahili. Sehemu D ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kutumia alama za uandishi katika lugha ya Kiswahili. Sehemu E ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma na kuelewa maudhui yaliyomo katika hadithi. Sehemu hizo tano zimetoka katika umahiri mkuu wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali* na *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiza au kulisoma*. Kila sehemu ilikua na swali moja (1) lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama kumi (10).

Jumla ya wanafunzi 1,681,769 walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne mwaka 2021. Waliofanya upimaji walikuwa.1,560,443 ambapo wanafunzi 1,326,573 sawa na asilimia 85.2 walifaulu.

Viwango vya ufaulu katika majibu ya wanafunzi vimegawanyika katika sehemu nne kulingana na alama walizopata. Kiwango hafifu ni kati ya alama 0-2.5, kiwango cha wastani ni 3-6, ufaulu mzuri 6.5-9.5 na ufaulu mzuri sana ni alama 10. Wanafunzi waliopata wastani, kiwango

kizuri na kiwango kizuri sana ndio waliohesabika kuwa wameweza kujibu maswali kwa usahihi. Hata hivyo, waliopata kiwango hafifu wameshindwa kujibu maswali kwa usahihi.

Aidha, katika taarifa hii, uchambuzi wa takwimu umewasilishwa kwa njia ya chati. Rangi mbalimbali zimetumika kuonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi kwa kila swali ambapo rangi nyekundu imetumika kuwakilisha kiwango hafifu cha ufaulu, yaani asilimia 0–33, rangi ya njano imetumika kuwakilisha kiwango cha wastani, yaani asilimia 34–66, rangi ya kijani imetumika kuwakilisha kiwango kizuri na kizuri sana mtawalia yaani asilimia 67–100.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Sehemu hii inachambua maswali yote yaliyoulizwa na majibu ya wanafunzi kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwa kila sehemu. Aidha, idadi na asilimia ya wanafunzi waliojibu vizuri na walioshindwa kujibu vizuri imeoneshwa katika chati. Hata hivyo, taarifa hii imeonesha sababu za ufaulu na kutofaulu kwa mwanafunzi kwa kila swali. Sampuli za majibu hafifu, wastani na mazuri zimetumika kuonesha viwango vya ufaulu kwa baadhi ya wanafunzi katika maswali.

### 2.1 Sehemu A: Imla

Sehemu hii ilikuwa na swali moja la imla. Wanafunzi walitakiwa kusikiliza kwa makini sentensi tano (05) walizosomewa kwa sauti kisha kuziandika kwa usahihi. Kila sentensi ilikuwa na maneno manne yenye alama nusu ($00^1/_2$) kwa kila neno. Kila sentensi ilikuwa na alama 2, hivyo kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri mkuu wa *kuwasiliana katika miktatha mbalimbali*.

Swali lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi katika kuandika sentensi kwa kuzingatia kanuni za uandishi kama vile, kuanza na herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi, alama ya mshangao, mkato, nukta pamoja na kutambua sauti mbalimbali katika matamshi ya silabi, maneno na sentensi. Swali hilo ni kama lifuatalo:

**Swali la 1**: **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) ______________________________

(ii) ______________________________

(iii) ______________________________

(iv) ______________________________


(v) ______________________________

Zifuatazo ni sentensi walizosomewa wanafunzi:

(i) Bibi yangu anaishi Kyela.
(ii) Ng’ombe wetu anaitwa Pato.
(iii) Juzi tulicheza mpira uwanjani.
(iv) Samani zina thamani mno.
(v) Babu atanunua kamba ndefu.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 1,560,443 (100%) waliofanya upimaji. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri kwani wanafunzi 1,310,605 sawa na asilimia 84.0 walijibu vizuri. Wanafunzi 324,524 sawa na asilimia 20.8 waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama zote 10. Aidha, wanafunzi 872,683 sawa na asilimia 55.9 walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5 kwani waliandika kwa usahihi maneno 13-19. Wanafunzi 113,398 sawa na asilimia 7.3 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6 ambapo

waliweza kuandika maneno 6-12. Wanafunzi 249,863 sawa na asilimia 16.0 walipata alama za kiwango hafifu kuanzia 0 hadi 2.5 kwa kuwa waliandika maneno 0-5 tu. **Chati Na. 1** inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.





**Chati Na. 1:** *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi waliofanya vizuri sana ni 324,524 sawa na asilimia 20.8 kwani waliweza kuandika maneno yote ishirini kwa usahihi.

Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kusoma na kuandika hivyo kuweza kubaini sauti zinazounda maneno yaliyosomwa na kuyaandika kwa usahihi huku wakizingatia kanuni za uandishi, matumizi ya herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi na maneno yaliyohitaji kuanza na herufi kubwa katikati au mwishoni mwa sentensi.

Vilevile, wanafunzi hao walikuwa na ujuzi wa kubaini na kuandika silabi zenye herufi mwambatano kama vile silabi *'kye'* kwenye neno "Kyela", silabi *'tha'* kwenye neno "thamani", silabi *'mba'* kwenye neno "kamba",


silabi *ng'o* na *'mbe'* kwenye neno "Ng'ombe". Maneno hayo ni miongoni mwa maneno yaliyounda sentensi za imla walizosomewa. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kusikiliza na kubaini matamshi ya herufi zinazounda maneno pamoja na kuzingatia kanuni za uandishi. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi sentensi zote tano kwa kuzingatia kanuni za uandishi hivyo kupata alama zote 10.


**Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Bibi yangu anaishi Kyela.
(ii) Ng'ombe wetu anaitwa Pato.
(iii) Juzi tulicheza mpira uwanjani.
(iv) Samani zina thamani mno.
(v) Babu atamunua kamba ndefu.

Kielelezo Na. 1.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1*

Hata hivyo, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 113,398 sawa na asilimia 7.3 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6 kwani waliweza kuandika maneno 6 hadi 12 kati ya maneno 20 yaliyounda sentensi zote tano. Wanafunzi hao, walizingatia kanuni za uandishi ingawa walishindwa kuandika baadhi ya maneno yenye silabi za herufi mwambatano.



1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) bibi yangu anauzhi kiela

(ii) ng ombe wetu anaitwa bato

(iii) Juzi tulicha pira uwalhani

(iv) samani zina samani muno


(v) babu atanunu kumbu defu

Kielelezo Na. 1.2: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 1*

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuandika baadhi ya maneno kwa usahihi na kushindwa kuandika maneno mengine. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika "*kiela*" kwenye neno la nne katika kipengele cha (i) badala ya Kyela, hata hivyo katika kipengele cha (ii) neno la kwanza aliandika "*ng ombe*"*.* Katika neno hilo hilo mwanafunzi aliacha nafasi kubwa kwenye silabi "ng'o" ambapo ni kinyume cha taratibu za uandishi wa neno linaloundwa na silabi zaidi ya moja. Aidha, katika neno hilo "ngombe" mwanafunzi aliacha alama ya mkato juu katikati ya fonimu *ng o* inayounda silabi ng'o ili kuunda neno ng'ombe. Vilevile, katika neno hilohilo alianza na herufi ndogo /ngo/ mwanzoni mwa sentensi. Katika kipengele cha (iii) neno la pili, la tatu na la nne alikosea na kuandika "tulicha" badala ya "tulicheza", "pira" badala ya "mpira" na aliandika "uwalhani" badala ya "uwanjani". Aidha, katika kipengele cha (iv) neno la tatu, mwanafunzi alishindwa kuandika kwa usahihi neno "thamani" na kuandika "samani" na katika kipengele cha (v) neno la pili na la nne alishindwa kuandika kwa usahihi neno "atanunua" na kuandika

“atanunu” na katika neno “ndefu” aliandika “defu”. Hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, wanafunzi 249,863 sawa na asilimia 16.0 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa sababu walishindwa kuandika kwa usahihi maneno waliyosomewa. Baadhi yao waliandika maneno bila kufuata kanuni za uandishi ambapo walichanganya herufi kubwa na ndogo, wengine hawakuacha nafasi kati ya neno moja na neno lingine, wengine walitenganisha silabi moja na silabi nyingine katika kuunda neno pamoja na kuanza na herufi ndogo mwanzoni mwa sentensi. Aidha, wanafunzi wengine walinakili maelekezo yaliyopo kwenye karatasi ya upimaji na kujaza sehemu iliyoachwa wazi. Hivyo, wanafunzi hao walipata alama za kiwango hafifu. Kielelezo Na. 1.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.



**Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(v)

Kielelezo Na. 1.3: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1*

Kielelezo Na. 1.3, kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye alijibu kinyume na matakwa ya swali kwa kuandika maneno bila kuzingatia kanuni za uandishi na kupata alama za kiwango hafifu.

## 2.2 Sehemu B: Umoja na Wingi

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano ambavyo vililenga kupima uelewa wa mwanafunzi kuhusu dhana ya umoja na wingi. Kila kipengele kilikuwa na alama mbili (2) na kufanya swali kuwa na jumla ya alama kumi (10).

**Swali la (2)** Andika wingi wa maneno yafuatayo kwa kuandika jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mto ____________________


(ii) Ukucha _________________

(iii) Ng'ombe ________________

(iv) Ufa ____________________


(v) Wembe ________________

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali* na lilimtaka mwanafunzi kuandika wingi wa maneno husika. Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,560,443 sawa na asilimia 100. Kiwango cha ufaulu katika swali kilikuwa kizuri kwa sababu wanafunzi 923,540 sawa na asilimia 59.2 waliweza kujibu vizuri swali hili. Wanafunzi 84,843 sawa na asilimia 5.4 waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 158,044 sawa na asilimia 10.1 walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 680,653 sawa na asilimia 43.6 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile, wanafunzi 636,928 sawa na asilimia 40.8 walipata alama za kiwango hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 2** inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa, wanafunzi 84,843 sawa na asilimia 5.4. walifaulu kwa kiwango kizuri sana kwani waliweza kuandika wingi wa maneno yote matano kwa usahihi na kupata alama zote 10. Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi waliofalu waliweza kubaini kuwa maneno ya Kiswahili yanaweza kubadilishwa kutoka maumbo ya umoja kuwa wingi kutokana na upatanisho wa kisarufi na ngeli za majina katika sentensi. Katika kipengele cha (i) neno mto walibaini wingi wake ni *mito*, katika kipengele cha (ii) ukucha wingi wake ni *kucha*, katika kipengele cha (iii) ng'ombe wingi wake ni *ng'ombe*. Aidha, katika kipengele cha (iv) ufa wingi wake ni *nyufa* na katika kipengele cha (v) wembe wingi wake ni *nyembe*. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha mwanafunzi aliyekuwa na umahiri wa maumbo ya umoja na wingi hivyo kujibu swali kwa usahihi.


2. Andika wingi wa maneno yafuatayo kwa kuandika jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mto Mito.

(ii) Ukucha Kucha.

(iii) Ng'ombe Ng'ombe.


(iv) Ufa Nyufa.

(v) Wembe Nyembe.

Kielelezo Na. 2.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2*

Kielelezo Na 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kubaini maumbo ya umoja na wingi kwa usahihi hivyo kupata alama zote 10.

Hata hivyo, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 680,653 sawa na asilimia 43.6 walipata alama za wastani. Wanafunzi hao walipata kuanzia 3 hadi 6 kwa kuwa waliweza kuandika wingi wa maneno 2 hadi 3 kati ya maneno 5. Ufaulu huo unaonesha kuwa, hawakuwa na maarifa ya kutosha ya kuelewa maumbo ya umoja na wingi ingawa waliweza kuandika baadhi ya maneno kwa usahihi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alishindwa kuonesha wingi wa neno wembe na kuandika “Ziwembe” badala ya “Nyembe”. Aidha, neno ukucha wingi wake aliandika “ukucha” badala ya “kucha”. Vilevile, neno ufa wingi wake aliandika “Ufa” badala ya “Nyufa”. Hata hivyo, wapo walioandika majibu yasiyokuwa na uhusiano na matakwa ya swali hivyo kubadili maana ya neno katika wingi. Mfano, neno wembe katika wingi “nyimbo”. Hivyo wanafunzi hao, hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini na kuandika maumbo ya umoja na wingi katika neno. Kielelezo Na. 2.2 (a) na (b) ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.



2. Andika wingi wa maneno yafuatayo kwa kuandika jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mto Mito


(ii) Ukucha ukucha

(iii) Ng'ombe Ng'ombe

(iv) Ufa ufa

(v) Wembe Ziwembe

Kielelezo Na. 2.2 (a): *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata vipengele viwili ambavyo ni (i) na (iii) hata hivyo kukosa katika kipengele (ii) (iv) na (v)*



2. Andika wingi wa maneno yafuatayo kwa kuandika jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mto Mito

(ii) Ukucha makucha

(iii) Ng'ombe Ng'ombe

(iv) Ufa kufa


(v) Wembe Nyimbo

Kielelezo Na. 2.2 (b): *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika majibu kuonesha wingi wa maneno ambayo ni tofauti na maneno aliyopewa*

Kielelezo Na. 2.2 (a) na (b), ni sampuli za majibu ya wanafunzi walioweza kuandika wingi kwa baadhi ya maneno kwa usahihi na kushindwa katika maneno mengine hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, wanafunzi 636,928 sawa na asilimia 40.8 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwani walishindwa kubaini usahihi wa maumbo ya umoja na wingi katika neno. Kwa mfano, katika kipengele cha (ii) neno Ukucha wingi wake aliandika *viukucha* badala ya *Kucha*. Pia, kipengele cha (v) Wembe wingi wake ameandika *viwembe* badala ya *Nyembe.* Vilevile, aliandika maneno kwa kuchanganya herufi kubwa na ndogo na neno hilo kulitungia sentensi. Mfano, neno ng'ombe katika kipengele cha (iii) wingi wake aliandika *Ng'oMBE waBaBaanakulamajani.*

Aidha, katika wingi wa neno ufa aliandika *usipo zi ufa utaJengaukuta.* Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kuelewa swali hivyo waliandika maneno nje ya matakwa ya swali husika ambapo walihusianisha neno walilopewa na makundi ya majina au matumizi na sauti za matamshi ya neno husika. Mfano neno Ukucha wingi wake aliandika "ukuta", katika neno Ng'ombe wingi wake aliandika "Mbuzi", neno Ufa wingi wake aliandika "kufa" na neno Wembe wingi wake aliandika "Jembe". Hivyo basi, majibu hayo yanaonesha kuwa wanafunzi hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maumbo ya umoja na wingi katika neno. Kielelezo Na. 2.3 (a) na (b) ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliyoshindwa kujibu swali kwa usahihi.



2. Andika wingi wa maneno yafuatayo kwa kuandika jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mto MItO


(ii) Ukucha VIÙKUCHA

(iii) Ng'ombe Ng'oMBE waBabaanakuLomajani

(iv) Ufa uSipo ziufa utaJengaukuta

(v) Wembe VIWEMbE

Kielelezo Na. 2.3 (a): *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2*



2. Andika wingi wa maneno yafuatayo kwa kuandika jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mto unguza

(ii) Ukucha ykuta

(iii) Ng'ombe Mbuzi

(iv) Ufa kufa

(v) Wembe Jembe


Kielelezo Na. 2.3 (b): *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2*

Kielelezo Na. 2.3 (a) na (b), kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi ambao walishindwa kuandika wingi wa maneno kwa usahihi kwa sababu hawakuwa na umahiri juu ya dhana ya maumbo ya umoja na wingi katika neno.

### 2.3 Sehemu C: Methali

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vinne (4) ambapo kipengele cha nne kimegawanyika katika sehemu mbili ndogo (a) na (b). Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali* na lililenga kupima matumizi ya methali na maana zake. Jumla ya alama katika swali hili ilikuwa 10 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 02.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,560,443 sawa na asilimia 100. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa sababu wanafunzi 652,857 sawa na asilimia 41.8 waliweza kujibu vizuri. Wanafunzi 11,630 sawa na asilimia 0.7 waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 4 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 63,175 sawa na asilimia 4.0 walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 578,052 sawa na asilimia 37.0 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile, wanafunzi 907,611 sawa na asilimia 58.2 walipata alama za kiwango hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 3** inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na**: 3: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3*

**Swali la 3:** Andika jibu sahihi kwa maswali yafuatayo:

(i) Bibi hulalamika kila siku anaibiwa fedha zake, siku moja alimkuta Chautundu anaiba fedha zake. Bibi atatumia methali ipi kumsuta Chautundu?

________________________________________

(ii) Utatumia methali ipi kumhimiza rafiki yako kufanya kazi kwa bidii? ______________________________

(iii) "Samaki mkunje angali mbichi" Methali hii ina maana gani?_____________________________________


(iv) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:

(a) Mdharau mwiba ____________________________

(b) Kilema si_______________________________

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 11,630 sawa na asilimia 0.7 walikuwa na kiwango kizuri sana cha ufaulu kwa kupata alama 10, kwani waliweza kujibu vipengele vyote vinne vya swali kwa usahihi. Wanafunzi hao, waliweza kuandika methali yenye maana sawa na maneno kwenye kipengele cha (i)–(iii) na kukamilisha methali kwa usahihi katika kipengele cha (iv). Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuwa methali huundwa na pande mbili zinazotegemeana kidhima na kimaana na kubainisha methali kutokana na mafunzo waliyopewa. Kwa mfano katika kipengele (i) mwanafunzi aliweza kubainisha methali iliyotumika kumsuta Chautundu aliyeiba fedha za bibi yake kwa kuandika "Siku za mwizi ni arobaini", katika kipengele (ii) aliweza

kubaini methali ya kuhimiza kufanya kazi kwa bidii kwa kuandika “Mchumia juani hulia kivulini”. Aidha, katika kipengele cha (iii) mwanafunzi alitoa maana ya methali *Samaki mkunje angali mbichi* kuwa *mfundishe mtu tabia nzuri angali akiwa mdogo* na katika kipengele cha (iv) aliweza kukamilisha methali (a) mdharau mwiba *mguu huota tende’* (b) Kilema si *ugonjwa*. Hivyo, wanafunzi hao walikuwa na weledi na maarifa ya kutosha ya kubainisha methali katika maneno walivyopewa na kukamilisha methali kwa usahihi. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote 4 vya swali kwa usahihi.



3. Andika jibu sahihi kwa maswali yafuatayo:

(i) Bibi hulalamika kila siku anaibiwa fedha zake, siku moja alimkuta Chautundu anaiba fedha zake. Bibi atatumia methali ipi kumsuta Chautundu?
Siku za mwizi ni arobaini.

(ii) Utatumia methali ipi kumhimiza rafiki yako kufanya kazi kwa bidii?
Mchumia juani hulia kivulini.


(iii) "Samaki mkunje angali mbichi." Methali hii ina maana gani?
Mfundishe mtu tabia nzuri angali akiwa mdogo.

(iv) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:
(a) Mdharau mwiba Guu huota tende.
(b) Kilema si Ugonjwa.

Kielelezo Na. 3.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3*

Kielelezo Na. 3.1, kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri kwa kufuata matakwa ya swali ambapo aliweza kubainisha methali katika vifungu vya maneno alivyopewa pamoja na kueleza maana ya methali na kukamilisha methali kwa usahihi.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 578,052 sawa na asilimia 37.0 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6 kwani waliweza kujibu vipengele 2 hadi 3 kwa usahihi. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kuandika methali kutokana na maneno walichopewa. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa maana na matumizi ya methali katika mazingira tofauti. Kwa mfano mwanafunzi mmoja katika kipengele cha (i) kilichomtaka kuandika methali ya kumsuta Chautundu ambaye anatabia ya wizi alijibu "hee! Chautundu kumbe ndio unaiba fedha zangu*"* badala ya kuandika "Siku za mwizi ni arobaini" ambalo ndilo lililokuwa jibu sahihi. Vilevile, katika kipengele cha (ii) kilichomtaka mwanafunzi kuandika methali inayohimiza kufanya kazi kwa bidii, na kujibu kuwa *rafiki yangu jitahidi kusoma kwa bidii* badala ya *Mchumia juani hulia kivulini/Jembe halimtupi mkulima/ Baada ya dhiki faraja* au *Mgaagaa na upwa hali wali mkavu*. Pia, katika kipengele cha (iii) kilichomtaka atoe maana ya methali "Samaki mkunje angali mbichi" na kujibu kuwa *mkimkunja ameshapikwa atakatika*. Hata hivyo, aliweza kukamilisha methali katika kipengele cha cha (iv) (a) na (b) kwa usahihi. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.



3. Andika jibu sahihi kwa maswali yafuatayo:

(i) Bibi hulalamika kila siku anaibiwa fedha zake, siku moja alimkuta Chautundu anaiba fedha zake. Bibi atatumia methali ipi kumsuta Chautundu?

heei Chautundu kumbe ndio unaeiba fedha zangu.

(ii) Utatumia methali ipi kumhimiza rafiki yako kufanya kazi kwa bidii?

Rafiki yangu jitahidi kusoma kwa bidii.

(iii) "Samaki mkunje angali mbichi." Methali hii ina maana gani?

ina maana samaki mkunje angali mbichi ni ukimkunja amesha kwatakatika

(iv) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:

(a) Mdharau mwiba Mguu huota tende.


(b) Kilema si Mgonjwa.

Kielelezo Na. 3.2: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 3*

Kielelezo Na. 3.2, kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi kipengele (iv) (a) na (b). na kushindwa kipengele (i), (ii) na (iii) na kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi 907,611 sawa na asilimia 58.2 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu na kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5. Wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi na maana ya methali katika miktadha mbalimbali. Wanafunzi hao walitoa majibu kinyume na matakwa ya swali kwa kuandika methali tofauti na vifungu vya maneno walivyopewa. Vilevile, walitoa maana ya methali husika ambazo sio sahihi na kukamilisha methali tofauti na swali

linavyotaka. Kwa mfano mwanafunzi mmoja katika kipengele cha (i) kilichomtaka kuandika methali ya kumsuta Chautundu ambaye anatabia ya wizi, aliandika kuwa *asie sikia la mkuu huvunjika guu.* Vilevile, katika kipengele cha (ii) kilichomtaka kuandika methali inayohimiza kufanya kazi kwa bidii aliandika kuwa *usikate tamaa endelea na masomo kwa bidii*. Aidha, katika kipengele cha (iii) kilichomtaka atoe maana ya methali "Samaki mkunje angali mbichi" aliandika kuwa *ukitumwa na mzazi wako usikatae inatakiwa uwende*. Pia, katika kipengele cha (iv) kilichomtaka kukamilisha methali (a) Mdharau mwiba aliandika *humchoma mwenyewe* na katika kipengele kidogo (b) Kilema si aliandika *mzigo*. Kielelezo Na. 2.3.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.



3. Andika jibu sahihi kwa maswali yafuatayo:

(i) Bibi hulalamika kila siku anaibiwa fedha zake, siku moja alimkuta Chautundu anaiba fedha zake. Bibi atatumia methali ipi kumsuta Chautundu?

asie sikia la mkuu huvunjika guu

(ii) Utatumia methali ipi kumhimiza rafiki yako kufanya kazi kwa bidii?

usikate ta maa Endelea na masomo kwa bidii

(iii) "Samaki mkunje angali mbichi." Methali hii ina maana gani?

ukitumwa na mzazi wako usikatae inatakiwa uwende

(iv) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:

(a) Mdharau mwiba humchoma mwenyewe

(b) Kilema si mzingo


Kielelezo Na. 3.3: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3*

Kielelezo Na. 3.3, kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata ufaulu hafifu kwa kuandika majibu yasiyokuwa na uhusiano na matakwa ya swali kutokana na kutokuwa na umahiri katika matumizi na maana ya methali mbalimbali.

## 2.4 Sehemu D: Matumizi ya Alama za Uandishi

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) ambapo kila kipengele kilikuwa na nafasi 2 za kujibu. Kila nafasi ilikuwa na alama 1, hivyo kufanya jumla ya alama 10 katika swali. Umahiri mkuu uliopimwa ulikuwa ni *Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma* na ulilenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kutumia alama za uandishi katika sentensi.

Wanafunzi waliojibu walikuwa 1,560,468 sawa na asilimia 100. Jumla ya wanafunzi 24,307 sawa na asilimia 1.6 waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 179,062 sawa na asilimia 11.5 walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 316,455 sawa na asilimia 20.3 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile, wanafunzi. 1,040,644 sawa na asilimia 66.7 walipata alama za kiwango hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 4** inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 4**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

**Swali la 4:** Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Afadhali___ mgeni amewasili____

(ii) Baba ameninunulia kalamu __ rula na daftari ___


(iii) Hodi___ je wenyeji wangu mpo___

(iv) Aka___ mimi sipendi utoro ___

(v) Mama ___ baba na kaka watasafiri kesho____

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 1,040,644 sawa na asilimia 66.7 walipata kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 2.5 kwani waliweza kujibu kipengele 1 tu au kushindwa kabisa. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kubaini alama za uandishi zinazotumika katika sentensi. Kwa mfano, wapo wanafunzi walioandika herufi katika nafasi husika kinyume na matakwa ya swali na wengine kuandika maneno kwenye nafasi iliyoachwa wazi kama vile, (i) *amefika* na *hapa*. Katika kipengele (ii) aliandika *penseli* na *ufuto*, katika kipengele cha (iii) aliandika *karibu* na *tupo.* Aidha, katika kipengele cha


(iv) *niambie* na *shuleni* na katika kipengele cha (v) aliandika *na* pamoja na *kutwa.* Kielelezo Na. 4.1: (a) na (b) kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi waliyoshindwa kuweka alama za uandishi katika sentensi.



4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Afadhali _A_ mgeni amewasili _B_.
(ii) Baba ameninunulia kalamu _D_ rula na daftari _R_.
(iii) Hodii _C_ je wenyeji wangu mpo _E_.
(iv) Aka _F_ mimi sipendi utoro _C_.
(v) Mama _B ._ baba na kaka watasafiri kesho _B_.

Kielelezo Na. 4.1 (a)*: Sampuli ya jibu baya katika swali la 4*



4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:


(i) Afadhali _amefika_ mgeni amewasili _hapa_
(ii) Baba ameninunulia kalamu _pensel_ rula na daftari _ufuk_
(iii) Hodii _karibu_ je wenyeji wangu mpo _tupo_.
(iv) Aka _niambie_ mimi sipendi utoro _shuleni_
(v) Mama _na_ baba na kaka watasafiri kesho _kutwa_

Kielelezo Na. 4.1 (b): *Sampuli ya jibu baya katika swali la 4*

Kielelezo Na. 4.1 (a) na (b), kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi waliyopata alama hafifu kwa kutokuwa na umahiri wa kutosha kuhusu alama za uandishi katika sentensi.

Aidha, wanafunzi 24,307 sawa na asilimia 1.6 walifaulu kwa kiwango kizuri sana kwani walijibu kwa usahihi vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Wanafunzi hao, waliweza kuweka alama za uandishi katika nafasi zilizokuwa wazi kwa usahihi, hivyo kufanya sentensi nzima kuwa

na mtiririko unaoleta maana. Kwa mfano, wanafunzi waliweza kubaini kuwa alama kituo/nukta inatumika mwishoni mwa sentensi. Aidha, waliweza kubaini kuwa alama ya mkato hutumika kuonesha pumziko dogo katika sentensi na kutenganisha vitu vilivyoorodheshwa. Vilevile, wanafunzi hao waliweza kubaini kuwa alama ya mshangao inatumika mahali ambapo kuna maelezo ya kushangaza, kusisitiza, kushtua, au kubeza. Sanjari na hayo, wanafunzi hao waliweza kubaini kuwa alama ya kuuliza hutumika katika maneno au sentensi zinazouliza maswali na mara nyingi hukaa mwishoni mwa sentensi. Kwa ujumla wanafunzi hawa walikuwa na umahiri wa kubaini alama za uandishi zinavyotumika katika sentensi za Lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote 5 vya swali kwa usahihi.


4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Afadhali __!__ mgeni amewasili __.__.

(ii) Baba ameninunulia kalamu __,__ rula na daftari __.__.

(iii) Hodii __!__ je wenyeji wangu mpo __?__.

(iv) Aka __!__ mimi sipendi utoro __.__.


(v) Mama __,__ baba na kaka watasafiri kesho __.__.

Kielelezo Na. 4.2**:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4*

Kielelezo Na. 4.2, kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuweka alama za uandishi kwa usahihi katika swali husika na kupata alama zote 10.

Hata hivyo, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 316,455 sawa na asilimia 20.3 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao waliweza kujibu vipengele 2 hadi 3 kwa usahihi kwani walikuwa na

umahiri wa wastani wa kutumia alama za uandishi katika sentensi. Wanafunzi hao walishindwa kuweka baadhi ya alama za uandishi kutokana na kushindwa kutofautisha alama ya mshangao pamoja na alama ya kuuliza. Hii inatokana na mazingira ya utokeaji wake hususani kwenye kupanda na kushuka kwa sauti (kiimbo) wakati wa utamkaji. Vilevile, wapo wengine walishindwa kutofautisha alama ya mkato na kituo hasa katika mazingira ya utokeaji na matumizi yake katika sentensi. Wengine waliandika maneno ya alama za uandishi badala ya kuweka alama za uandishi na wengine kuweka alama za funga semi na fungua semi. Kielelezo Na. 4.3 (a) na (b) ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliyopata alama za wastani.


4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Afadhali " mgeni amewasili " .


(ii) Baba ameninunulia kalamu , rula na daftari ? .

(iii) Hodii , je wenyeji wangu mpo . .

(iv) Aka , mimi sipendi utoro . .

(v) Mama , baba na kaka watasafiri kesho ? .

Kielelezo Na. 4.3 (a): *Sampuli ya jibu lenye alama za wastani katika swali la 4*


4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:

(i) Afadhali ____ mgeni amewasili ____

(ii) Baba ameninunulia kalamu ____ rula na daftari ____ .

(iii) Hodii ! je wenyeji wangu mpo ? .

(iv) Aka ! mimi sipendi utoro mshangao .

(v) Mama ____ baba na kaka watasafiri kesho mkato

Kielelezo Na. 4.3 (b): *Sampuli ya jibu lenye alama za wastani katika swali la 4*

Kielelezo Na. 4.3 (a) na (b), kinaonesha sampuli ya jibu la wanafunzi waliyoweza kujibu kwa usahihi vipengele 3 na kushindwa vipengele 7 hivyo kupata alama za wastani.

## 2.5 Sehemu E: Ufahamu

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma*. Swali lilipima umahiri wa mwanafunzi wa kusoma hadithi na kujibu maswali yaliyofuata.

**Swali la 5:** Soma kwa makini hadithi ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

*Hapo zamani za kale Kanga na Kuku walikuwa marafiki sana. Wote waliishi kwa binadamu. Kuku alikuwa na tabia ya uchoyo. Kuku alikuwa na sindano nzuri ya kushonea nguo. Kila siku Kanga alipojaribu kuazima sindano, Kuku alikataa katakata. Siku moja Kanga aliiba sindano ya kuku akaenda kuificha porini.*

*Kuku aliporudi aliitafuta sindano yake kila mahali lakini hakuiona. Alianzisha ugomvi mkubwa Sana. Wakati wanapigana, Kuku alichukua kalamu mezani kisha akampigia Kanga. Kwa bahati mbaya wino wa kalamu ulivuja na kumdondokea Kanga. Kuku aliendelea kumdondoshea Kanga wino mpaka ukaisha. Ndiyo maana hadi leo Kanga ana madoadoa na Kuku anaparua ardhini kutafuta sindano yake.*

**Maswali**

(i) Kuku na Kanga waliishi wapi?

_______________________________________________

(ii) Nani alikuwa na sindano ya kushonea nguo?

_______________________________________________

(iii) Sindano ilipoibiwa ilifichwa wapi?

_______________________________________________


(iv) Hadithi hii inahusu nini?

_______________________________________________

(v) Hadithi hii inatoa funzo gani?

_______________________________________________

Jumla ya wanafunzi 1,560,443 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani wanafunzi 1,166,508 sawa na asilimia 74.8 ndio waliofanya vizuri. Wanafunzi 300,896 sawa na asilimia 19.3 waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 479,454 sawa na asilimia 30.7 walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 386,158 sawa na asilimia 24.7 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile, wanafunzi 393,960 sawa na asilimia 25.2 walipata alama za kiwango hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 5** inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.





**Chati Na. 5**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5*

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 1,166,508 sawa na asilimia 74.8 walifaulu kwa kiwango kizuri. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote 5 na kupata alama 10 kwani walikuwa na umahiri wa kusoma hadithi na kubaini maudhui yaliyomo. Kwa mfano, katika kipengele cha (i) kilichomtaka mwanafunzi aeleze mahali walipoishi Kanga na Kuku, walitoa jibu kuwa, *kuku na kanga waliishi kwa binadamu.* Kipengele cha (ii) kilichomtaka mwanafunzi aeleze kuwa nani alikuwa na sindano ya kushonea nguo, walijibu kuwa ni *kuku*. Aidha, kipengele cha (iii) kilimtaka mwanafunzi aeleze sindano iliyoibiwa ilifichwa wapi, walitoa jibu kuwa ilifichwa *porini*.

Pia katika kipengele cha (iv) kilimtaka mwanafunzi aeleze hadithi inahusu nini, wengi walijibu kwa usahihi na kuandika hadithi hii inawahusu *kuku na kanga*. Vilevile, kipengele cha (v) kilimtaka mwanafunzi aeleze funzo linalopatikana katika hadithi, walijibu kwa usahihi kuwa hadithi hii inatufundisha *tusiwe wachoyo* na wengine walijibu *tusiwe wezi*. Kwa ujumla majibu hayo yanaonesha kuwa

wanafunzi walikuwa na umahiri wa kutosha wa kusoma hadithi na kuelewa maudhui yaliyomo katika hadithi husika. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu maswali kwa usahihi kutokana na hadithi aliyoisoma.



**Maswali**

(i) Kuku na Kanga waliishi wapi?

Kuku na Kanga waliishi kwa binadamu.

(ii) Nani alikuwa na sindano ya kushonea nguo?

aliekuwa na sindano ya kushonea nguo ni kuku.

(iii) Sindano ilipoibiwa ilifichwa wapi?

Sindano ilipoibiwa ilifichwa porini.

(iv) Hadithi hii inahusu nini?

Hadithi hii inahusu Kuku na Kanga.

(v) Hadithi hii inatoa funzo gani?


Hadithi hii inatufundisha kusiwe wachoyo.

Kielelezo Na. 5.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5*

Kielelezo Na. 5.1, kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri vipengele vyote 5 kwa sababu alikuwa na umahiri wa kusoma hadithi na kufahamu maudhui yaliyomo na kupata alama zote.

Hata hivyo, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 386,158 sawa na asilimia 24.7 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 2 hadi 3 vya swali. Aidha, walishindwa kujibu vipengele vingine kutokana na kukosa umahiri wa kusoma na kubaini wazo kuu katika hadithi husika. Kwa

mfano, mwanafunzi mmoja alishindwa kujibu kipengele cha (iv) kilichomtaka kueleza hadithi inahusu nini alijibu kuwa *hapozamani za kale* badala ya kuandika ‘hadithi inahusu Kanga na Kuku’. Aidha, katika kipengele cha (v) kilichomtaka mwanafunzi aeleze funzo linalopatikana katika hadithi, alijibu kuwa *kuku alikuwa mchoyo’*. Hata hivyo, mwanafunzi aliweza kujibu kwa usahihi katika kipengele (i), (ii) na cha (iii). Kwa ujumla majibu hayo yanaonesha kuwa wanafunzi walikuwa na umahiri wa wastani wa kusoma na kubaini maudhui katika hadithi waliyosoma. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu baadhi ya vipengele kwa usahihi.



**Maswali**

(i) Kuku na Kanga waliishi wapi?
Kwa binadamu

(ii) Nani alikuwa na sindano ya kushonea nguo?
Kuku

(iii) Sindano ilipoibiwa ilifichwa wapi?
porini

(iv) Hadithi hii inahusu nini?
hapo zamanizakale

(v) Hadithi hii inatoa funzo gani?
Kuku alikuwamchoyo

*Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya jibu la wastani katika swali la 5*

Kielelezo Na. 5.2, kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi kipengele cha (i), (ii) na (iii) na kushindwa kipengele (iv) na (v) na kupata alama ya wastani.

Aidha, wanafunzi 393,960 sawa na asilimia 25.2 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwani walipata alama kuanzia 0 hadi 2.5. Wanafunzi

hao, hawakuwa na umahiri wa kusoma na kuelewa maudhui yaliyomo katika hadithi. Baadhi yao walishindwa kujibu kwa usahihi kutokana na kutojua kusoma na kuandika. Uchambuzi unaonesha kuwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali husika. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika kipengele cha (i) kilichomtaka aeleze kuku na kanga waliishi wapi, aliandika *NYUMBANI*, katika kipengele cha (ii) kilichomtaka aeleze nani alikuwa na sindano ya kushonea nguo, aliandika *MTU*. Aidha, katika kipengele (iii) kilichomtaka mwanafunzi aeleze mahali ilipofichwa sindano alijibu *HOSPITARINI*. Pia, katika kipengele cha (iv) kilichomtaka mwanafunzi aeleze hadithi aliyoisoma inahusu nini, alitoa jibu kuwa inahusu *MASWALI*. Vilevile, katika kipengele cha (v) kilichouliza hadithi inatoa funzo gani, na kujibu FUNZO RAERIMU. Kwa ujumla majibu yanaonesha kuwa wanafunzi hawakuwa na umahiri wa kusoma na kubaini maudhui katika hadithi waliyosoma hivyo kushindwa kujibu kwa usahihi maswali yote. Kielelezo Na. 5.3 (a) na (b) ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi waliyoshindwa kujibu swali kwa usahihi.

**Maswali**

(i) Kuku na Kanga waliishi wapi?

NYUMBANI

(ii) Nani alikuwa na sindano ya kushonea nguo?

MTU

(iii) Sindano ilipoibiwa ilifichwa wapi?

HOSPITARINI


(iv) Hadithi hii inahusu nini?

MASWALI

(v) Hadithi hii inatoa funzo gani?

FUNZO BAERIMU

Kielelezo Na. 5.3 (a): *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5*


**Maswali**

(i) Kuku na Kanga waliishi wapi?

poRini mbuga zowanyama

(ii) Nani alikuwa na sindano ya kushonea nguo?

msho na cheRt hani

(iii) Sindano ilipoibiwa ilifichwa wapi?

ili pichwa nyumbani

(iv) Hadithi hii inahusu nini?

hadithi hi afusu kuwega

(v) Hadithi hii inatoa funzo gani?

hiRatoa funzo zuRi

Kielelezo Na. 5.3 (b): *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5*

Kielelezo Na. 5.3 (a) na (b) kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu vizuri kutokana na kukosa umahiri wa kusoma na kuelewa mawazo yaliyotolewa katika hadithi kwa usahihi na wengine kutojua kusoma na kuandika.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Upimaji wa somo la Kiswahili umehusisha umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali na Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilosikiliza au Kulisoma*. Upimaji huu ulikuwa na maswali matano ambayo yalipima uwezo wa wanafunzi wa kusikiliza na kuandika matamshi ya silabi, maneno na sentensi (Imla), umahiri wa kutambua maumbo ya umoja na wingi, kukamilisha na kutoa maana ya methali, kuonesha alama za uandishi katika sentensi, pia kusoma na kujibu maswali kutoka kwenye hadithi.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali* ulikuwa na maswali 3, swali la 1, 2 na 3 na ulikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 61.66. Swali la 1 lilikuwa na ufaulu mzuri wa asilimia 84.0 ambapo swali hilo lilikuwa na asilimia kubwa ya ufaulu kuliko maswali yote. Swali la 2 na 3 yalikuwa na ufaulu wa wastani. Swali la 2 lilikuwa na asilimia 59.2 na swali la 3 lilikuwa na asilimia 41.8. Hata hivyo, umahiri wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilosikiliza au Kulisoma* ulikuwa na maswali 2, swali la 4 na swali la 5 na umahiri huo ulikuwa na ufaulu wa wastani, wa asilimia 54.05. Aidha, swali la 4 lilikuwa na ufaulu hafifu kwa kuwa na asilimia 33.3 ya ufaulu kuliko maswali yote. Swali la 5 lilikuwa na ufaulu mzuri wa asilimia 74.8 mtawalia. Taarifa hizi za uchambuzi zimeambatanishwa kwenye kiambatisho cha pekee.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa ufaulu wa jumla wa Upimaji wa Kitaifa Darasa la Nne katika somo la Kiswahili 2021 ni mzuri sana. Wanafunzi 1,326,573 sawa na asilimia 85.2 walifaulu katika upimaji huo kwa kupata alama 10 hadi 50. Wanafunzi hao walikuwa na uwezo wa kusikiliza na kuandika matamshi ya silabi, maneno na sentensi (Imla), kutambua maumbo ya umoja na wingi, kukamilisha na kutoa maana ya methali, kuonesha alama za uandishi pamoja na kusoma na kujibu maswali kutoka kwenye hadithi.

Aidha, jumla ya wanafunzi 233,870 sawa na asilimia 14.8 walikuwa na utendaji hafifu. Wanafunzi hao walishindwa kujibu maswali kwa ufasaha kutokana na changamoto mbalimbali kama vile: kushindwa kumudu stadi za kusoma na kuandika, kuwapo kwa athari ya lugha mama, kushindwa kuelewa matakwa ya swali na kukosa umahiri wa

kutambua alama sahihi za uandishi katika sentensi pamoja na kushindwa kujua maumbo ya umoja na wingi katika neno.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Pamoja na ufaulu mzuri sana wa somo la 01 Kiswahili, juhudi za makusudi hazina budi kuzingatiwa ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa Darasa la Nne kwa miaka ijayo. Juhudi hizo ni kama ifuatavyo*:*

(a) Walimu wahakikishe wanafunzi wanaweza kutamka na kuandika sauti za herufi mwambatano kama vile, *ky, ng'o, mb, nj, tw, ng'w, nyw, gh, py, nz, lw, pw* na *sw* katika silabi, sentensi na habari fupi. Vilevile, waweze kutofautisha matamshi ya maneno yenye herufi *s* na *th, z* na *dh*, *v* na *f* na *l* na *r* ili kuwajengea umahiri wa kusoma na kuandika sentensi za Imla katika umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali.

(b) Walimu wahakikishe wanafunzi wanakuwa na uwezo wa kubaini maumbo ya umoja na wingi katika neno kwa kutumia picha, michoro na vitu halisi, ili waweze kuelewa kwa urahisi umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali.

(c) Walimu watilie mkazo ufundishaji wa umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali hususani katika methali mbalimbali za lugha ya Kiswahili. Aidha, watumie matini, picha au chati zinazoonesha maumbo ya methali na maana zake katika kufundishia.

(d) Walimu watumie picha au chati zinazoonesha alama mbalimbali za uandishi kama vile, alama ya mshangao, alama ya kuuliza,

alama ya kituo, alama ya mkato na alama ya funga semi na fungua semi katika sentensi au habari fupi.

(e) Walimu wahakikishe wanafunzi wanapata misingi madhubuti ya kusoma ili kuwajengea uwezo katika kutumia misamiati mipya katika lugha ya Kiswahili. Aidha, wawapatie wanafunzi vifungu vya habari/hadithi vilivyopo katika vitabu vyao vya kiada na kuwapa maelekezo ya kusoma na kujibu maswali watakayoulizwa. Lengo ni kupima uelewa wa matini waliyoisoma wanafunzi.

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

## ULINGANIFU WA UFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2020 NA SFNA 2021

| Na. | Umahiri Mkuu | Upimaji 2020 | | | | Upimaji 2021 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1 | 85.1 | 77.13 | Vizuri | 1 | 84.0 | 61.66 | Wastani |
| | | 2 | 85.7 | | | 2 | 59.2 | | |
| | | 4 | 60.6 | | | 3 | 41.8 | | |
| 2. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 3 | 69.6 | 60.40 | Wastani | 4 | 33.3 | 54.05 | Wastani |
| | | 5 | 51.2 | | | 5 | 74.8 | | |